

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



MKUU WA TAKUKURU MKOA

Mtaa wa Uzunguni,

S.L.P 37,

37101 SHINYANGA,

Tanzania.

Simu: (028) 2762630

Nukushi: (028) 2763358

SHINYANGA 03 Julai 2020.

TAARIFA KWA UMMA.

TAKUKURU SHINYANGA INAMSHIKILIA JOSEPH JONAS TASIA KWA KUKUTWA NA DOTI MIA SITA ZA VITENGE VYENYE NEMBO YA CHAMA CHA MAPINDUZI NA VYA KAWAIDA.

TAKUKURU mkoa wa Shinyanga katika ufuatiliaji wa vitendo vya Rushwa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Viongozi, mnamo tarehe 29/06/2020 majira ya saa tatu usiku katika mtaa wa Mwasele B nyumbani kwa JOSEPH JONAS TASIA ilikamata doti 600 za vitenge vyenye nembo ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na vya kawaida vikiwa vimehifadhiwa nyumbani kwake jambo ambalo linaashiria kuwa vilikuwa vinaandaliwa kutumika katika kufanya ushawishi kwa wapiga kura.

Aidha uchunguzi wa TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga umebaini kwamba JOSEPH JONAS TASIA ambaye ni mfanyabiashara wa usafiri wa magari madogo TAXI hana duka na wala hafanyi biashara ya kuuza vitenge.

Katika mahojiano na Maafisa wa TAKUKURU mkoa wa Shinyanga baada ya mtuhumiwa kukamatwa na mzigo huo ameshindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza kuhusiana na mzigo husika na hata nyaraka za manunuzi ya mzigo huo alizowasilisha hazijitoshelezi na hivyo kuongeza mashaka juu ya uhalali wa vitenge hivyo.

Uchunguzi wa kina bado unaendelea ili kubaini iwapo vitenge hivyo vilikuwa ni kwa ajili ya kuhusika na vitendo vya Rushwa katika uchaguzi ujao au ni kwa ajili ya kufanya biashara katika msimu huu wa kuelekea katika Uchaguzi Mkuu wa Viongozi.

Taarifa rasmi itatolewa mara baada ya uchunguzi kufichua ukweli uliojificha.

ONYO

TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga inawaonya watu wote wenye nia ya kutaka kutumia taarifa zozote za uchunguzi zinazofanyiwa kazi na ofisi hii kwa nia ya kujinufanisha kisiasa na kwamba kitendo hicho ni kuingilia uchunguzi unaondelea na ni kosa la jinai. Hivyo atakayefanya hivyo atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Imetolewa na H.M.Mussa Mkuu wa TAKUKURU (M) Shinyanga.

*Barua zote zitumwe kwa Mkuu wa TAKUKURU Mkoa, Mtaa wa Uzunguni, S.L.P. 37,
37101SHINYANGA. Unaweza pia kuwasiliana nasi kwa njia ya simu ya Bure 113,
instagram: takukuru.tz, Facebook: TakukuruTz, Twitter: TAKUKURU.TZ, Online TV:
TAKUKURUTV*